

Nambari ya Mtahiniwa _____

S.M.Z.

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR
MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA
127 DINI KIISLAMU

MUDA: SAA 2.00

JUMANNE 22 NOVEMBA 2017

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu TANO (5) A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, B, C Na chagua maswali MATATU (3) kutoka sehemu D, swali la NANE (8) ni lazima. Pia chagua swali MOJA (1) tu kutoka sehemu E.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Andika majibu ya mtihani katika nafasi zilizowekwa.

KWA MATUMIZI YA USAHIHISHAJI TU		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
JUMLA		

Mtihani huu una kurasa 13 zenye maandishi

SEHEMU A: QUR-AN NA TAFSIRI (Alama: 20)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Chagua jibu sahihi na uandike herufi yake kwenye sanduku liliopo chini.

i. Sura inayompwekesha Allah (S.W) ni sura

A: Nasri

B: Fat-ha

C: Ikhlaasi

D: Fat-hi

ii. Maana ya Tajwidi kilugha ni:-

A: Uzuri.

B: kuleta jambo kwa vizuri.

C : Kuipa kila herufi haki yake.

D: Usahihi wa mambo.

iii. Waliokasrikiwa katika suratul-fatiha ni

A: Mayahudi.

B: Manaswara.

C: Manaswara na Mayahudi .

D: Mayahudi na Makafiri.

iv. Suratul-fatiha ina aya :-

A: 7

B: 6

C: 8

D: 5

v. Bismillahi ni aya katika Suratul

A: Mauuna

B: Tawbah

C: Fat-ha

D: Fat-hi

vi. Herufi za Idgham ni:-

A: 5

B: 6

C: 4

D: 7

vii. Ni vizuri zaidi kwa mwenye kuchukua msahafu awe:

A: Muislamu.

B: Muislamu balegh na mwenye akili.

C: Balegh na mwenye akili.

D: Muislamu na msafi.

viii. Asili ya mwanadamu ni mwenye kukanusha. Ukweli huu unathibiti katika suratul:-

A: Zil-zala.

B: Aadiyati.

C: Takathuru.

D: Qaariya.

ix. Neno "مُنْعَكَيْنَ" katika suratul-Bayyina linamaana ya:-

A: Wenye kushikilia rai zao.

B: Hawajielewi

C: Wajuzi sana kifikra.

D: Wenye kiburi kutokana na rai zao.

x. Zil - zala maana yake ni:

A: Kugeuka kwa ardhi

B: Kukasirika kwa ardhi .

C: Kuzunguka kwa ardhi

D: Kutetemeshwa kwa ardhi

JIBU:

i.	ii	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

2. a) Panga Tafsiri za aya zifuatazo kwa usahihi wake.

i. Shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa.

ii. Ataingia moto wenye muwako mkubwa.

iii. Imeangamia mikono miwili ya Abulahabi nae amekwisha angamia

iv. Mkewe mchukuzi wa kuni.

v. Haitamfaa mali yake wala alivyovichuma.

i. _____

ii. _____

iii. _____

iv. _____

v. _____

b) Tafsiri aya zifuatazo:-

أ- وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْقَارِعَةُ

ب- الَّذِي أَنْقَضَ
ظَهْرَكَ.

ج - إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا.

c) Lete mafunzo mawili yanayopatikana katika suratul zilzala.

SEHEMU B: TAWHIIDI (Alama: 20)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

3. Chagua jibu kutoka Orodha 'A' kwa kulinganisha kifungu cha maneno kutoka Orodha 'B'. Andika herufi ya jawabu katika sanduku.

Orodha 'A'	Orodha 'B'
i. Alama za mnafiki	a. Mfumo wa maisha
ii. Fatani	b. Majina ya Mwenyezi Mungu (S.W).
iii. Dini	c. Kujitenga na dunia
iv. Sema, muombeni Allah (S.W)	d. Kuweka mwenza wa Allah (S.W)
v. Utawa	e. Anapoaminiwa hufanya hiana.
vi. Ushirikina	f. Kufuata muongozo wa Allah (S.W)

vii. Kuamini Allah (S.W)	g. Marejeo na hesabu yao ni juu yetu
viii. Kuamini Malaika	h. Hana mshirika wala msaidizi
ix. Kuamini mitume ya Allah (S.W)	i. Wengine wametajwa katika Qur`an
x. Kuamini siku ya mwisho	j. Kugombanisha waumini
	k. Hawaasi amri za Allah (S.W)
	l. Kukaa faragha

JIBU:

i.	ii	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

4. Andika herufi "K" kwa ibara iliyokuwa sahihi na herufi "S" kwa ibara isiyokuwa sahihi. Kisha andika herufi husika katika sanduku liliopo chini.

- Ziko aina kuu tatu za dini.
- Kuchinja kwa ajili ya shetani ni imani ya kishirikina.
- Malaika Jibrilu (A.S) ni malaika mtukufu kuliko wote.
- Mitume iliyotajwa ndani ya Qur-ani nusu yao wamepewa vitabu.
- Nguzo za Ihsani ni mbili.
- Haifai kuomba dua kwa kutumia majina ya Mwenyezi Mungu.
- Inapendeza kwa Muislamu anapoaminiwa kufanya khiyana.
- Hakuna mtume anaeitwa Ilyasau.
- Nabii Issa (A.S) hajafa.
- Mwenye kusikia ni jina la Mwenyezi Mungu.

JIBU:

a.	b.	c.	d.	e.	f.	g.	h.	i.	j.

SEHEMU C: HADITHI (Alama: 20)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii

5. Uislamu umeweka wazi nidhamu na heshima za kaka katika makaazi mbali mbali yakiwemo nyumbani, sokoni, barazani na hata njiani. Orodhesha haki tano (5) za mwenye kukaa njiani zilizoelezwa katika Uislamu.

i. _____

ii. _____

iii. _____

iv. _____

v. _____

6. a) Lete tafsiri hadithi ifuatayo kwa lugha ya Kiswahili:-

قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ (اتَّقِ اللَّهَ حَيْثُ مَا كُنْتَ وَأَتَّبِعِ السَّبِيلَ الْحَسَنَ تَمَحُّهَا
وَخَالِقِ النَّاسَ بِخُلُقٍ حَسَنٍ) (رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ)

- b) Ainisha mafunzo mawili yatokanayo na hadithi iliopo juu.

SEHEMU D: FIQHI NA MAADILI (Alama: 30)

Jibu maswali MATATU (3) katika sehemu hii likiwemo suala la NANE (8).

7. Jaza mapengo yafuatayo kwa kuweka maneno yaliyokosekana:
- i. Hija ni faradhi kwa kila _____ aliye na uwezo na hutakiwa kuhiji mara _____ katika umri wake.
 - ii. Miongoni mwa masharti ya hija ni _____ na _____.
 - iii. Zakka ni nguzo ya _____ katika uislamu.
 - iv. Sala ya _____ ni faradhi kifaya.
 - v. Mtume Muhammad (S.A.W) amesema swala ni _____ ya dini mwenye kusimamisha swala _____ dini.
 - vi. Funga ya _____ ni _____ kwa ya kila Muislamu.
8. Jaza kwa usahihi nafasi zilizoachwa wazi.
- a) Mwanamme wa Kiislamu hatakiwi kuvaa vazi lenye _____
 - b) Mwanamke wa Kiislamu anatakiwa _____ mwili _____ isipokuwa uso na viganja viwili.
 - c) Mwanamme wa Kiislamu hatakiwi kuvaa nguo za aina ya _____ na mapambo ya _____.
 - d) Vazi la mwanamke wa Kiislamu lisiwe lenye kuonesha _____ wake.
 - e) Mwanamke wa Kiislamu hatakiwi kujifananisha na _____ muislamu katika _____.
 - f) Uasharati husababisha maradhi mbali mbali yakiwemo _____ na _____.

- 9 . Kusimamisha sala ni nguzo ya pili ya kiislamu. Orodhesha nguzo tano za sala.

10. Bi Salma alikumbuka kwamba hakupaka maji kichwani wakati wa kutia udhu, wala hakuelekea kibla wakati anaswali. Muelekeze Bi Salma hatua ya kuchukua ili swala yake iwe sahihi.

Nambari ya Mtahiniwa _____

SEHEMU E :TAREKHE (Alama: 10)

Jibu suali MOJA (1) tu katika sehemu hii:

11. a. Elezea maana ya Muhajirina na Answare.
- b. Taja masahaba wawili (2) wa Kianswari na wawili (2) wa Muhajirina.
- c. Bainisha faida ziliyopatikana kutokana na udugu wa Kiislamu baina ya Muhajirina na Answare

Nambari ya Mtahiniwa _____

This image shows a full page of blank, lined paper. It features approximately 20 evenly spaced horizontal black lines across its entire width, providing a template for handwriting practice or general note-taking. The margins are consistent on all sides.

Nambari ya Mtahiniwa _____

12. Eleza mateso walioyapata waislamu wa Mwanzo kabla ya kuhamia Uhabeshi.

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

[illegible]

Ukurasa wa **13** kati ya **13**